

Jina:

Nambari:

Shule:

Sahihi

Tarehe:

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA 3

FASIHI

OCT/NOV 2010

MUDA :SAA 2 ½

MTIHANI WA TATHMINI WA SOUTH LINK **KIDATO CHA TATU**

Kiswahili

Karatasi ya 3

MAAGIZO:

- *Jibu maswali **manne** pekee.*
- *Swali la **kwanza** ni la **lazima**.*
- *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Ushairi, Tamthilia, Hadithi fupi na Fasihi simulizi.*
- *Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja***
- *Karatasi hii ina kurasa 6 zilizopigwa chapa.*
- *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karsatasi hii zimepigewa chapa sawasawa na kuwa maswali yotr yamo.*

SEHEMU A

RIWAYA.

S.A MOHAMMED: Utengano

1. LAZIMA

“Mkubwa kabisa ni mwananchi. Umma ndio mkubwa kabisa na umma umeshautenda vya kutosha.”

- a) Eleza muktadhda wa dondoo hili. (alama 4)
- b) Onyesha vile mzungumziwa alivyotendea umma mabaya. (alama 12)
- c) Fafanua sifa za anayesema. (alama 4)

SEHEMU YA B:

TAMTHILIA

KITHAKA WA MBERIA: Kifo Kisimani.

Jibu swali la 2 au la 3

- 2 Kwa kutolea mifano maridhawa, tetea kauli kuwa ‘ Butangi ni mojawapo ya nchi za kiafrika zina zoendelea. (ala. 20)
- 3. “ Nimesema yeye ni mhalifu kutokakana na vitendo vyake vya kiuharibifu,. Kwani wataka nikueleza mara ngapi?”
 - a) Eleza Muktadha wa dondoo hili (ala ma 4)
 - b) Ni matendo gani ya kinyama aliyoyafanya msemaji wa maneno. (alama 6)
 - c) Ukitoa mifano faafu, onyesha uzalendo wa aliyeambiwa maneno haya. (ala ma 6)
 - d) Anayenukuliwa katika dondoo ana umuhimu gani katika tamthilia ya kifo Kisimani? (alama 4)

SEHEMU C:

HADITHI FUPI

K.W WAMTILA: Mayai Waziri wa Maradhi.

Jibu swali la 4 au la 5

- 4. Jamii inayorejelewa katika hadithi ya Mayai Waziri wa Maradhi ni kielelezo mwafaka cha yanayoendelea katika nchi nyingi barani Afrika.

Fafanua ukweli wa kauli hii huku ukitoa mifano hadithini. (alama 20)

- 5. “ Huoni mabadiliko yoyote katika tabia na mienendo yake?
 - a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (ala ma 4)
 - b) Kuna mabadiliko gain. Katika tabia na mienendo ya anayerejewa? (alama 4)
 - c) Fafanua mambo yanayochangia tabia hii. (alama 4)
 - d) Jadili sifa za msemewa. (alama 4)

SEHEMU D:

FASIHI SIMULIZI

6. a) i) Miviga ni nini? (alama 2)
ii) Taja sababu za kufanyika kwa miviga (alama 4)
iii) Eleza umuhimu wa miviga (alama 10)
- b) Fafanua istilani za fasihi simulizi zifuatazo (alama 4)
i) Maghani.
ii) Mighani.

SEHEMU E

USHAIRI.

7. Soma shairi lifuatala kisha ujibu maswali.

UHABA.

Uhaba una ndwele mbi, una ndwele mbi uhaba,
Uhaba huleta dhambi, mtu hutamani kwiba,
Uhaba hupiga kambi, lango hutia bawaba,
Haba hwondoa haiba, ya kila kilo kamili

Uhaba hasa kipato, mtu hali akashiba,
Kipato kikae shoto, mtu akilubaluba,
Uhaba una majuto, uhaba una misiba
Haba hwondoa haiba, ya kila kilo kamili.

Uhaba ni udhaifu, kukosa hata akiba,
Uhaba hutia hafu, haujazi na kibaba,
Uhaba hutiwa dufu, kwa riziki kuliziba,
Haba hwondoa haiba, ya kila kilo kamili.

Uhaba na udhalili, katiti haina twiba,
Uhaba japo akili, umepungua mkoba,
Akili kuwa kalili, unipele ka kwenye miba,
Haba hwondoa haiba, ya kila kilo kamili.

Uhaba hata wa penzi, wapendano kwa huba,
Uhaba una simanzi, uhaba matilaba,
Uhaba huleta ganzi, kuyunguka ushuba,
Haba hwondoa haiba, ya kila kilo kamili.

Uhaba japo wa afya, hama dumu ya kuzaba,
Maisha kukuogofya, kushukwa shukwa na waba,
Uhaba hata wa chafya, kupiga yagobagoba,
Haba hwondoa haiba, ya kila kilo kamili.

Haba pia wa elimu, asoelewa kitaba,

Hili nalo hafahamu, hata kupima miraba,
Uhaba unadhulumu, hupunja watu si haba,
Haba hwondoa haiba, ya kila kilo kamili.

Awe fundi wa mitindo, zile myema wasemayo,
Ya kumbwaya na msondo, na ufundi mwingineyo,
Si ufundi ni urundo, madhali anacho choyo,
Mtu dhaifu wa moyo, husuda kwake kikao.

Na awe bingiso wa lugha, na mengi yatakiwayo,
Ya hadhara na faragha, na kila mali iwayo,
Si bingwa bali ni Nyagha, madhali mtu wa payo,
Mtu dhaifu wa moyo, husuda kwake kikao.

Awe hodari kujenga, kila banda ajengayo,
Bingwa wa safu kupanga, mapao na kombamoyo,
Si fundi bali mjinga, madahli ana matayo,
Mtu dhaifu wa moyo, husuda kwake kikao.

Maswali.

- a) Eleza bahari kuu ambazo zimetumiwa na mshairi (alama 4)
b) Chambua shairi kwa kuzingatia muundo. (alama 4)
c) Mtunzi ametumia uhuru gani katika kutunga shairi hili? Toa mifano kwa kila moja (alama 2)
d) Andika ubeti wa tatu katika lugha ya nathari. (alama 4)
e) Ni mbinu gani za sanaa zilizoshirikishwa katika shairi hili? (alama 2)
f) Eleza maana ya maneno yafuatayo katika shairi (alama 4)
 i) Mbi
 ii) Kalili
 iii) Twiba
 iv) Nyagha